

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129
Nukushi: 026 -2322126

Baruapepe: km@michezo.go.tz
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali- Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

Dodoma,
15 Novemba, 2023

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA WASANII WHOZU, BILLNAS NA MBOSSO KWA SHARTI LA KULIPA FAINI NA KUSOGEZWA MBELE RUFAA YA MSANII NEY WA MITEGO

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, (Mb) amewaondolea adhabu ya kifungo cha kutojikusisha na shughuli za muziki hapa nchini Wanamuziki wa Bongofleva **Whozu**, **Billnas** na **Mbosso** na kuwaagiza walipe faini ili waweze kuruhusiwa kufanya kazi za sanaa, kufuatia kukutwa na makosa ya ukiukaji wa kanuni zilizomo kwenye Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili ya Kazi za Sanaa wa mwaka 2023.

Uamuzi huo umefikiwa katika kikao cha pamoja kati ya Wizara na Wanamuziki hao cha kusikiliza rufaa iliyowasilishwa na mwanamuziki **Whozu**, ambaye video ya wimbo wake "**Ameyatimba**" uliowashirikisha wasanii **Mbosso** na **Billnas** ulifungiwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Novemba 2, 2023 kwa kuwa na maudhui yanayokiuka maadili kinyume na kanuni ya 25(6), (j) pia kuonesha vitendo vya unyanyasaji, ukatili na udhalilishaji wa Utu wa mwanamke kinyume cha kanuni ya 25(6)-(f).

Katika kikao hicho kilichofanyika Novemba 14, 2023 jijini Dar es Salaam, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amemuagiza mwanamuziki Whozu alipe faini ya shilingi milioni 5 kutoka shilingi milioni 3 za awali alizotakiwa kulipa kutokana na mwanamuziki huyo kurudia makosa na kukaidi adhabu ya awali aliyopewa na BASATA.

Aidha, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amemuondolea kifungo cha miezi 6 cha kutojikusisha na shughuli za muziki hapa nchini alichokuwa amepewa mwanamuziki huyo kutokana na video yake na kumwagiza kuiondoa video hiyo kwenye mitandao yake ya Kijamii kama alivyotakiwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Kwa upande wa mwanamuziki **Mbosso** ambaye alikiri kosa la kushiriki katika maudhui ya wimbo huo ambayo ni kinyume cha kanuni za maadili, ametakiwa kulipa faini ya shilingi milioni 3 na kufutiwa adhabu yake ya kufungiwa kwa miezi 3 huku mwanamuziki **Billinas** ametakiwa kulipa faini ya shilingi milioni 1 na kuondolewa adhabu ya kifungo cha miezi 3 aliyokuwa amepewa ya kutojikusisha na shughuli za muziki hapa nchini.

Mhe. Waziri Dkt. Damas Ndumbaro ameliagiza Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lichukue hatua dhidi ya wataalamu wanne (4) waliohusika katika kufanikisha kukamilika na kutolewa kwa wimbo huo ambao ni Mtayarishaji (Producer), Muongozaji (Director), Mwandishi wa Wimbo na Mtayarisha maudhi (Content creator) kwa kuwa wamehusika dhidi ya kosa lililotendwa na wasanii hao.

Katika hatua nyingine Waziri Dkt. Damas Ndumbaro ameahirisha kusikiliza rufaa ya Mwanamuziki wa Bongofleva **Ney wa Mitego** ya kupinga kufungwa kwa wimbo wake wa '**Amkeni**' kutokana na msanii huyo kutangulia kulipeleka shauri lake kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri Dkt. Damas Ndumbaro amewaasa wasanii hao na wengine nchini waendeleo kutumia vizuri ubunifu wao na kufuata taratibu zilizoainishwa katika mwongozo wa uzingatiaji maadili katika kazi za sanaa nchini ili Watanzania waendeleo kuburudika na kunufaika na kazi zao zinazozingatia maadili ya Mtanzania.

Imetolewa na;-



Aron Msigwa

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI